

MCHANGO WA MOHAMMED KIJUMWA KATIKA FASIHI YA KISWAHILI

Beja S. Karisa

1.0 Utangulizi

Muyaka, Ali bin Nassir, Mwalimu Sikujua na Mohammed Kijumwa ni mionganini mwa waandishi wa kazi za fasihi ambao wametoa mchango mkubwa katika kuvyaza na kuendeleza fasihi ya kale ya Kiswahili. Madhumuni ya makala haya ni kueleza mchango wa Mohamed Kijumwa katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa jumla hasa kwa mwelekeo wa nadharia ya uamilifu. Nadharia ya uamilifu iliasisiwa na Bronislow Malinowski na Radcliffe Brown (Abraham, 1993) kama nadharia iliyojikita katika utamaduni. Walisema “Uamilifu ni kazi ambayo kitu hufanya katika mfumo ambamo kitu hicho kimo”. Kwa mujibu wa usemi huu uamilifu hurejelea utekelezaji wa jukumu maalumu katika jamii. Ni kwa misingi hii ambapo makala haya yanachambua mchango wa Mohammed Kijumwa katika kuvyaza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili.

2.0 Historia ya Kijumwa

Mohammed Kijumwa au kwa ukamilifu Mohammed Bin Abubakar Bin Omar Kijumwa aliiishi baina ya mwaka 1855 na 1945. Alizaliwa na kulelewa na mama yake, Mwana Kamari, katika kisiwa cha Lamu. Ijapokuwa alikuwa mzawa wa Lamu yeye mwenyewe alikuwa akijitambulisha kama Mswahili mwenye asili ya Kiarabu kama asemavyo katika ubeti wa utenzi ufuatao:

Nimetengeza muyinga
Musioyua kutunga
Mimi Kijumwa muanga
Asili al-Arabiya

Kijumwa aliinukia kama mtoto mwenye nidhamu, na alisafiri mara kwa mara na mamake mpaka Unguja, na kuwahi kuhiji Makka mara nne. Kijumwa alikuwa na vipaji vya aina mbalimbali za sanaa kama vile sanaa ya utunzi wa mashairi, tenzi na nyimbo. Aliweza kutunga nyimbo papo kwa papo na pia kuweza kukariri beti nyingi kwa moyo. Aidha alikuwa na kipaji cha sanaa ya

uchongaji (useremala), mkono wa maandishi na uundaji w^a ala za muziki. Kijumwa alizaliwa na kulelewa katika mazingira ya Kiswahili na dini ya Kiislamu. Aliishi nyakati ambazo ukanda wote wa Mwambao wa Afrika Mashariki na visiwa vyake ulikuwa chini ya himaya ya Usultani wa Oman ambaeo ulikuwa na makao yake makuu katika kisiwa cha Unguja. Nyakati hizo, kulikuwa na uhusiano na mwingiliano wa kijamii na kiuchumi kwa Waswahili wote katika eneo la ukanda wa Mwambao ambalo lilichukuliwa kama jumuiya moja ya Waswahili. Kwa hali hii, kulikuwa na uhuru wa kutembea na kuishi mahali popote katika Mwambao wa Afrika Mashariki. Uhuru huu ulimwezesha Kijumwa kutembea na kuishi Unguja na kujifunza mengi, hasa kuhusu muziki. Mapenzi yake ya nyimbo na ala za muziki yalishika moto hasa alipozuru Unguja na Uarabuni mwaka 1875 akiwa na mama yake ambaye pia alikuwa ni mtunzi. Kijumwa alipenda zaidi mashindano ya nyimbo na ngoma katika maisha yake kwani baada ya kifo cha mama yake (1882), aliasi mambo ya chuoni (madrasa) na kushikilia mambo ya ngoma. Mwelekeo wa ngoma na nyimbo ndio uliotawala maisha yake na kumfanya ajiingize katika ulimwengu wa muziki hadi kifo kilipomchukua.

Baada ya kifo cha mamake, Kijumwa alizuru Uarabuni (1884) kwa madhumuni ya kujifunza mahadhi ya muziki wa Kiarabu, na aliporudi, alikuwa amehitimu katika nyimbo za Kiarabu na hata katika kutengeneza ala za muziki kama vile kinanda (Abouegl, 1984). Inasemekana kuwa Kijumwa ndiye mtu wa kwanza kuanzisha ngoma ya kinanda katika Lamu. Mohammed Kijumwa baada ya kpalilia kipawa chake cha utunzi aliibuka kama manju wa kusifika. Umahiri wake katika nyimbo na ngoma ulionekana hasa katika mashindano ya ngoma mbalimbali, akishindana na Bwana Zena ambaye awali alikuwa mwanafunzi wake katika utunzi wa nyimbo. Katika mashindano kama haya, Kijumwa, siku zote, aliibuka mshindi. Weledi wake wa utunzi na uimbaji ulimfanya Kijumwa atunukwe na Sultan Hamoud wa Unguja alipozuru Lamu, mwaka 1901. Kwa siku zote hamsini Sultan alizokuwa Lamu, Kijumwa ndiye aliyekuwa akimtumbuiza. Alimtungia Sultani nyimbo mpya kila siku, tena za papo kwa papo, akimsifu. Sultan Hamoud aliporudi Unguja, alimchukua Kijumwa ili akaungane na watumbuizaji wake wengine. Kijumwa alikwenda Unguja, akawa mtumbuizaji wa Sultan Hamoud mpaka Sultan alipokufa (Abouegl, 1984).

Kijumwa alipokuwa Unguja, alijiunga na kikundi cha ngoma kutoka Misri kilichoitwa Ikhwan-al-safa, ambacho kilikuwa kimekuja kwa madhumuni ya kumtumbuiza Sultani. Kikundi hiki kutoka Misri, inasemekana, ndicho kilicholeta ngoma ya Taarab Unguja, mpaka mwaka 1905 ambapo Waswahili wenyewe waliunda kikundi chao cha Taarab. Alipokuwa Unguja, Kijumwa alipalilia kipaji chake cha utunzi wa nyimbo mpaka akawa manju wa taarabu na

mwalimu wa kuwafunza wengine kama vile Mbaruk ambaye baadaye alikuja kuungana na Siti binti Saad na kuunda kikundi chao cha taarab huko Unguja. Aliporudi Lamu mwaka 1908, Kijumwa alianzisha ngoma ya taarab Lamu na akafufua mashindano ya ngoma na manju wa maeneo mengine.

3.0 Mchango wa Kijumwa katika fasihi

Tunaweza kugawanya mchango wa Mohammed Kijumwa katika sehemu tatu muhimu. Kwanza, tunaweza kuuona mchango wake katika fasihi simulizi ya Kiswahili, pili katika utunzi wa fasihi andishi na tatu, tunaweza kuuona mchango wake akiwa mwalimu wa watunzi.

3.1 Mchango wa Kijumwa katika Fasihi Simulizi

Mtu anaposikia matamshi "Fasihi Simulizi," akili yake hutua mara moja juu ya hadithi na vitendawili na kusahau nyimbo na ngoma ambazo ni sehemu muhimu katika fasihi simulizi. Nyimbo ni utanzu wa mashairi simulizi katika fasihi simulizi. Nyimbo kama mashairi ni kazi ya sanaa inayoshughulikiwa katika fasihi simulizi. Hivyo basi, Kijumwa, kama manju wa Lamu, ana mengi aliyochangia katika nyimbo na mashairi ya Kiswahili kwa jumla kulingana na jinsi alivyopendelea nyimbo na mashindano ya ngoma.

3.2 Nyimbo na Ngoma

Kijumwa alikuwa mtunzi wa nyimbo za ngoma za aina mbali mbali ambazo alikuwa akishindana na manju wengine kama vile Bwana Zena. Mashindano haya yaliipa uhai na maendeleo fasihi simulizi hasa katika utanzu wa ngoma, nyimbo na mashairi na kuvyaza aina mpya za ngoma. Mchango wa Kijumwa katika upande wa nyimbo na ngoma unaonekana hasa pale alipoanzisha ngoma mpya mionganoni mwa jamii ya Waswahili. Baadhi ya ngoma mpya alizozianzisha ni ngoma ya Dhili, ngoma ya Washa na Kinanda huko mjini Lamu. Pia ndiye aliyeleta ngoma ya taarab Lamu kutoka Unguja mwaka 1908 (Abouegl, 1984). Mbali na ngoma hizi, Kijumwa alipendelea sana ngoma za beni na gungu.

Kijumwa alichangia kwa kiasi kikubwa katika utanzu wa mashairi ya jamii ya Waswahili wa Lamu. Alianzisha mashindano ya ngoma hizo alizozianzisha na zile zilizokuweko tayari mjini Lamu.

Mashindano mengi ya ngoma hizi yalikuwa msukumo mahsus kwa Kijumwa, hasa katika utunzi wa nyimbo. Kila ngoma ilihitaji nyimbo zake, na kila shindano lilihitaji nyimbo mpya. Umbuji huu ulimfanya Kijumwa asifike mpaka siku moja Sultan Hamoud alipokuwa ametembelea Lamu alimtunuka Kijumwa na akamtaka aende naye Unguja ili akajumuike na manju wengine katika kumtumbuiza yeche Sultani. Mkusanyaji wa nyimbo za Kijumwa yasema kuwa

alikusanya nyimbo 200, na nyingi ni zile ambazo hazikumbukwi tena (Abouegl,1984).

Ngoma ya Dhili ni mfano wa ngoma alizozianzisha Kijumwa. Hii ilikuwa ni ngoma iliyochezwa katika sherehe za mashindano yaliyochukua juma moja. Kawaida ilichezwa mara moja kila mwaka. Sherehe hizi zilikuwa zikifanywa katika majahazi yasiyo tanga. Majahazi hayo yalikuwa yakirembwa kwa marembo mbalimbali kama vile maua, bendera na nguo. Waimbaji walijimba na kucheza, huku wakitia madoido, kama vile sanamu. Majahazi huwa baharini, ilhali watazamaji huwa ufukoni. Madhumuni ya sherehe hizi ilikuwa ni kutakia heri na ufanisi mwaka mpya katika kilimo na uvuvi. Mashindano yalikuwa baina ya mikao. Kwa mfano, kulikuwa na mkao wa Mkomani chini ya Kijumwa na mkao wa Nidhamu chini ya Bwana Zena .

Ngoma ya Washa ni mfano mwengine wa ngoma iliyoanzishwa na Kijumwa. Mwanzo ilipobuniwa, ngoma hii iliitwa ngoma ya Kukata Shingo, baadaye ikaja kuitwa Goma la Njiwa, kisha ndiyo ikaja kuitwa ngoma ya Washa. Kijumwa aliendelea mashindano ya ngoma ya Washa mpaka miaka ya 1930 alipotangaza kustaafu kwake kwa sababu yauzee.

Beni ni aina nyininge ya ngoma iliyobuniwa na Kijumwa mwaka 1900. Kulikuwa na mikao miwili ya ngoma hii. Mkao wa kwanza ukiwa chini ya Bwana Zena uliitwa Kingi, na mkao wa pili ukiwa chini ya Kijumwa ulikuwa ukiitwa Skochi. Mikao hii miwili ilikuwa ikishindana sana mpaka mwaka 1925. Awali, mkao wa Kingi ulikuwa na nguvu kuliko Skochi kwa sababu ulikuwa ukipata vifaa vya muziki kutoka ng' ambo kupitia kwa mkao wa Kingi wa Mombasa. Lakini baadaye, mkao wa Kingi wa Lamu uligawanyika ukawa mikao miwili - mmoja chini ya Bwana Zena ukiitwa Kingi na mwengine ukiwa chini ya Subiriana ukiitwa Kambaa. Baadaye, mkao wa Subiriana uliungana na mkao wa Kijumwa - hapo ndipo mkao wa Kijumwa ulikuwa na nguvu zaidi ya mkao wa Bwana Zena. Mashindano yaliedelea hadi Bwana Zena alipokufa mwaka 1933. Mashindano yalifufuka mwaka 1934 wakati Bi. Zuhura alipochukua hatamu ya uongozi wa mkao wa Kingi. Mashindano yalikuwa makali, hasa katika kuchokozana, mpaka viongozi wa dini ya Kiislamu wakaitaka serikali ikataze mashindano hayo. Mashindano yalikatazwa lakini baadaye yalikubaliwa tena.

Kijumwa alijibu malalamiko ya viongozi wa dini kwa kutunga wimbo ufuatao ijapo hakufaulu:

Mumekwisha kutwandama, tungawa tu waumbufu,

Mwaliliani nyama, nanyi ni wasitirifu?

Beni halina karama, hatutaki masharifu.

Ngoma ya Beni iliendelezwa hata baada ya kifo cha Kijumwa, lakini baadaye ilikatazwa kabisa mwaka 1963 baada ya uhuru.

4.0 Maudhui ya mashairi ya Kijumwa

Mohammed Kijumwa alitunga nyimbo nyingi juu ya mambo mbalimbali katika jamii ya Waswahili wa Lamu. Mazingira na matukio ndyo yaliyokuwa msingi na msukumo wa utunzi wake. Alikuwa akitunga nyimbo zake kujokana na tukio aliloliona wakati ule ule.

Nyimbo za Kijumwa zilimulika matukiv ama hali halisi ya maisha ya Waswahili katika mazingira ya Lamu. Tunaweza kuseni, kwa ufupi, kuwa nyimbo zake zilihusu kazi, utamaduni na hali ya maisha ya Waswahili kisiasa na kiuchumi.

5.0 Shughuli za Waswahili

Baadhi ya shughuli za Waswahili ambayo zimezungumziwa katika nyimbo za Mohammed Kijumwa ni uvuvi, ukulima, ugemza na biashara. Vile vile kuna vyombo mbali mbali ambavyo hutumiwa na Waswahili katika shughuli zao. Baadhi ya vyombo ambavyo vinadokezewa katika tungo za Kijumwa ni zana za kazi walizotengeneza kama vile pondo za kuvulilia na majembe ya kulimaa. Ithibati ya baadhi ya shughuli za Waswahili tunaipata katika baadhi ya beti za nyiripo alizotunga Kijumwa kwa ngoma mbalimbali. Kwa mfano:

Ugema

Na unazo tatu tama kikwambia utalia
Kwanda huisi kusma, la pili huna tabia
Enenda zako mgama, ni lipi nalokutia

Uvuvi

Siweke zitendo isizo maana
Ukikosa pondo ivuvi hapana

Biashara

Ni udhia tajunuu, ukitojua kunena
Hayakuwa naaiuu, yambo umezolifana
Sasa huzanyatambuu, mahamra hupijana.

Katika beti zilitodolewa hapo juu shughuli za ugema, uvuvi na biashara kama vile kuuzataanbuu na mahamra, zaonyeshwa ni baadhi ya shughuli zilitokithiri katika nyakati za Kijumwa na mpaka sasa bado baadhi yazo zinaendelezwa.

6.0 Utamaduni wa Waswahili

Utamaduni ni baabu ya maudhui aliyoshughulikia sana Kijumwa. Katika nyimbo zake, amehifalihii utamaduni katika ndoa, mapenzi, uganga na dini - hasa dini

ya Kiislamu ambayo imeathiri sana utamaduni wa Waswahili. Beti tulizokusanya zinadhahirisha kuhifadhiwa kwa mambo haya:

Ndoa

Maneno yako hukomi, wataka nami ninene
Kuo si kwanda mimi , watangulie wengine
Kwa hadithi ya Mtumi, sheria ni wake wane.

Mapenzi

Wako currati aima, simuwate maridhia
Utakalo kwangu jama, nambia hela nambia
Chungu kimevuja nyama, mtuzi umebakia.

Takwambia nave utuwe makini
Hakupenda nave uyue ya ndani
Ito likiona moyo hutamani.

Kuhusu ndoa, Kijumwa atujulisha ya kwamba kulingana na athari za dini ya Kiislamu, Waswahili waliruhusiwa kuo wake wanen. Katika mapenzi, Kijumwa atuonyesha ya kwamba kupendana na kuachana ni jambo la kawaada na kwamba aghalabu yule anayeachwa katika mapenzi huwa na jukumu la kumbembeleza mwenzake.

Wanawake

Wanawake wa kisasa, mbovu hali zao
Wakikosa pesa, hawana pumbao
Kheri kuwakosa, kama kuwa nao.

Kijumwa anawalaamu na kuwaonya wanawake wa Lamu wa nyakati zake kwamba walikuwa wamependa fedha mno zaidi ya mapenzi yenye. Jambo ambalo lilihatarisha uhusiano kati ya mwanamke na mwañamme.

Dini na Imani

Dunia haikaliki, kuna miba hunitoma
Na akhira hakwendeki, siyatanguliza wema
Kikwambia husadiki, kwekeza sikio kufuma.

Moyo wangu una nini, hulia kucha na kutwa
Humshiriki shetani, kwa yambo usolipata
Aliyekufa ni nani, kilio kikamleta.

Beti hizi zinadhihirisha kwamba Kijumwa na watu wa Lamu kwa jumla walikuwa na imani ya dini na kwamba kumshiriki shetani ni jambo litakaloelekeza miyo yao akhera ambako hakwendeki.

Hali ya Maisha

Kwa jumla Kijumwa alikuwa akielekezwa sana na matukio na hali ya maisha ya Waswahili wa Lamu katika utunzi wake. Hivyo basi, nyimbo zake zinajikita katika uyakinifu wa hali halisi ya maisha ya Waswahili wa Lamu wa nyakati zake. Baadhi ya nyimbo ambazo tunewahi kuzipata zinadhihirisha hali ya utumwa na ubwana katika maisha ya Waswahili wa nyakati hizo. Vilevile zinaonyesha mashindano ya ngoma – jambo alilopendelea sana Mohammed Kijumwa. Zifuatazo ni baadhi ya beti za nyimbo zinazotupatia ithibati ya madai yetu:

Utumwa na ubwana

Ya Wahidu Subuhana

Ya Suridu Saidana

Sayyidi Hamudu maulana

Tumekuya kwako bwana

Kuamkia sute watumwa

Sayyidina Hamudu maulana

Bwana meipenda Amu yetu

Kisa meipenda dola yetu

Watumwa kumshashia ndilo letu.

Huu ni wimbo rimojawapo kati ya nyimbo alizotunga Kijumwa kwa madhumuni ya kumtumbuiza Sultan Hamoud alipotembelea Lamu kama tulivyoeleza katika Historia ya Kijumwa. Wimbo huu unadhihirisha kinagaubaga kwamba nyakati za Kijumwa kulikuwa na maisha ya kitabaka ya utumwa na ubwana katika eneo la Lamu.

7.0 Mashindano ya Ngoma na Kujigamba

Mashindano ya ngoma na nyimbo ni jambo alilopenda sana Kijumwa mpaka ikamlazimu aache kwenda madrasa baada ya kufa mama yake. Nyingi ya nyimbo zake zimedhihirisha mashindano ya ngoma yaliyokuwa yakifanyika Lamu kati ya maeneo tofauti tofauti, Kijumwa akiwa kiongozi wa mmoja wa mikao hiyo. Kujigamba ni tabia ya watunzi. Kijumwa hakutindikiwa na jambo

hili kama manju wa Lamu, aliyeshindana sana na Bwana Zena. Hapa kuna baadhi ya vifungu vinavyotonga majigambo ya Kijumwa kwa wapinzani wake:

Lipunguze omo tanga, kuna kusi la khatari
Waniyua si muinga, kwa tepe henda Misiri
Upetepo tia nanga, imbali nawe bandari

Nahudha punguza tanga, baharia wamechoka
Ukiiza nami simo, hasa Kilifi tashuka
Utabishaye mfumo, na mai yamerundika.

Huwa na yangawa hufaani
Watambuzi tambuani
Mlio wa chuwa utamdhuru nyani?

Siasa

Hali ya kisiasa ni moja ya mambo aliyoshughulikia Kijumwa. Katika baadhi ya beti za nyimbo zake anatumulikia utawala wa kisultani na wa kikoloni. Kwa mfano, ule wimbo wa Sultan Hamoud uliotolewa hapo juu unadhihirisha utumwa na ubwana. Aidha Kijumwa anatufahamisha kuwa kulipa kodi lilikuwa ni jambo lililoendelezwa na serikali ya Lamu wakati huo. Beti zifuatazo zinadhihirisha jambo hili pamoja na kuwaonya wenzake dhidi ya kutosalimu amri, ila wamwachie mwenyezi Mungu:

Sifanyeni masikhara, serikali ina nguvu
Walimwengu majura, wasifanye ushupavu
Zitawapata khasara, muzidishapo uwovu

Nikupiga hodi hodi, kila siku mara tatu
Waekeni mashahidi, kama waekao watu
Mungu tusalimu kodi, majumba hayana zitu.

8.0 Mtindo wa nyimbo za Kijumwa

Nyimbo za Kijumwa, kama nyimbo za watanzi wengine, zilikuwa na mishororo mitatu katika kila kifungu (ubeti). Nyingi ya nyimbo hizo zilikuwa na mizani 16 kila mishororo, ijapokuwa kuna mishororo kadhaa ambayo ilikuwa na mizani 15. Kila ubeti ulikuwa na vina vya ndani na vya nje. Hata hivyo, kuna nyimbo nyingine ambazo zilikuwa na mizani kati ya 8 na 12. Nyimbo kama hizi zilikuwa fupi na zilikuwa na vina vya nje pekee. Kwa mfano:

Twambie nawe utuwe makini
Nakupenda nawe uyue ya ndani
Ito likiona hutamani.

Lugha

Kijumwa alitumia lugha fasaha na ya kitamathali kwa usanii mkubwa. Usanii wa kutumia mafumbo ulichangia mno katika kufanya nyimbo za Kijumwa zipendwe zaidi ya nyimbo za manju wengine wa kumbo lake. Baadhi ya beti za nyimbo zinazoonyesha mafumbo na ufundi wa lugha hasa katika utumiaji wa lugha ya kitamathali ni hizi zifuatazo:

Iwapo u mtatuzi, tatuwa kitetenecho
Ukiweke wazi wazi, kama kitatushiyecho
Utatuwapo muyuzi, unambie hiki ndicho.

Ubeti huu unaonyesha jinsi Kijumwa alivyokuwa mweledi katika kuwafumbia watunzi wenzake hasa, Bwana Zena, ambaye alikuwa mpinzani wake katika ngoma na nyimbo hadi kufa kwake. Mfano mwingine wa nyimbo zilizofumba ni:

Bui wangu mwenye sifa, ndoo nikupe khabari
Nikupe la maarifa, la mila na desturi
Kizima na chenye ufa , ni kipi chenye khatari

Siwezi tena matata, nenda kaketi utuwe
Kwani huzipanga zita, hatuziisi mwandowe
Mpiga konde ukuta, huumiza mkonowe

Mbali na kutumia mafumbo, Kijumwa alitumia methali katika utunzi wake kama tunavyoona katika ubeti wa pili wa vifungu viliviyotangulizwa hapo juu. Kijumwa akiwa mzawa wa Lamu, nyimbo zake zote zilikuwa katika lahaja ya Kiamu.

Ujuzi wake wa lugha na kipawa chake cha utunzi vilifanya Kijumwa aonekane kama ‘Muyaka wa Lamu.’

9.0 Mchango wa Kijumwa katika fasihi andishi

Kijumwa aliishi nyakati za utawala wa kisultani na baadaye wazungu walipotia guu pwani ya Afrika Mashariki na kuona utumwa ukiendelea, walipendelea kuliingilia suala hili la utumwa. Kishaye, watumwa walianza kuachiliwa huru tangu tarehe 1.11.1889 mpaka mwaka 1897, baada ya mkataba kati ya sultani na

serikali ya Uingereza. Kutoka mwaka 1890, pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa chini ya utawala wa Waingereza baada ya maelewano na Wajerumani na Waarabu wa Oman. Ili kutawala pwani na Kenya kwa jumla, Uingereza ililetia viongozi na wawakilishi wa mfalme wa Uingereza. Hawa walikuwa magavana, wakuu wa wilaya na wa mitaa. Wetgine walikuwa wamishenari. Hawa walifuatiwa na watafiti wa Uingereza na nchi nyingine kama vile Ujerumani. Baadhi ya viongozi, wamishenari na watafiti hawa, walijiingiza katika utafiti wa fasihi ya Kiswahili. Ni wakati huu ndipo tunaona umuhimu mkubwa wa Mohammed Kijumwa katika fasihi andishi ya Kiswahili. Tunaweza kuugawa umuhimu wake katika sehemu tano. Kwanza, Kijumwa alinakili tenzi, mashairi na hadithi baada ya kuzitafsiri kwa Kiswahili na kuziingiza kazi hizo za sanaa katika fasihi ya Kiswahili. Pili, alinakili tenzi na mashairi yaliyotungwa na watunzi wenzake waliomtangulia kama vile Sayyid Abdalla bin Ali bin Nassir (1720-1830). Tatu, alitunga mashairi yake yeeye mwenyewe na kuyahifadhi katika maandishi. Jukumu hili alilifanya baada ya kuombwa afanye hivyo na wale wazungu ambao walijitia utafiti wa fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya wazungu hao ni:

Alice Werner, Prof Meinhof, E. Dammann, J.W.T Allen, William Hichens, Capt. Stigand, J.K.Knappert, Dr. Buettner na H.E Lambert.

Nne, Kijumwa alitunga mashairi, tenzi na hadithi. Tano, Kijumwa aliwafunza wengine kutunga mashairi.

10.0 Kutafsiri Tenzi na Hadithi za Kiarabu

Tenzi na hadithi za Kiarabu ziliingizwa katika fasihi ya Kiswahili. Kazi hizi za fasihi, awali, zilikuwa katika lugha ya Kiarabu. Kijumwa alitafsiri nyingi ya kazi hizi za fasihi kwa Kiswahili na kuwapa wazungu waliochapisha katika vitabu mbali mbali. Mfano wa utenzi wa Kiarabu alioutafsiri Kijumwa ni “Utendi wa Barsisi na Hasina.” Huu ni utenzi uliotoka katika kitabu cha Kiarabu kiitwacho *Al – Mustalraf Fi Kulli Fannin Mustadharf* kilichoandikwa na Muhammad Ibn Ahmad al – Ibshaihi. Hiki ni kitabu chenye tenzi na hadithi za Kiarabu ambacho Kijumwa, yasemekana, alikisoma sana. Utensi huu wa “Barsisi na Hasina” alimpa W. Hichens ambaye aliuchapisha.

Kwa upande wa hadithi, Kijumwa alitafsiri hadithi za Kiarabu kama vile Hadithi ya Kozi na Ndiwa. Hii ni hadithi ya Kiarabu ambayo awali, ilikuwa ikiitwa “ Kissat Musa Ma’ah al Bazi wa’ L- Hamani.” Hii ni hadithi inayofanana na ile ya Mtume Musa. Aidha Kijumwa alitafsiri vitabu vyingine kama vile *al- Arbaini Hadithi, al-Saifu al -Qati: na Kitab al-Madih* – Kitabu cha Kiarabu ambacho kinamsifu mtume Mohammad S.A.W.

Umuhimu wa Kijumwa katika shughuli za kutafsiri tungo za Kiarabu hadi Kiswahili unaelezwa pia na Harries (1950) anaposema:

“Kitabu hiki, *Dichtungen in der Lamu – Mundart der Suaheli*, hakijapewa ukipaumbele katika nchi hii (Britain) lakini ni kitabu kizuri kabisa cha mkusanyiko wa tendi ambazo zimewahi kuchapishwa. Kina tendi saba zenye tafsiri ya kuaminika, na washairi waliotafsiri ni kama Muhammad (Kijumwa Abubakar bin Umar) ambao ni Manju wa ushairi wa Kiswahili.”

Kupitia tafsiri za Kijumwa, tenzi na mashairi ya Kiarabu yaliingizwa katika fasihi ya Kiswahili.

Kunukuu Tenzi na Mashairi

Mbali na tafsiri, Kijumwa alitekeleza pia shughuli za unukuzi wa tungo ambazo zilikuwa awali zimetungwa na Waswahili na kuandikwa kwa Kiswahili wakitumia hati za Kiarabu. Kijumwa alinukuu tungo hizo na kuziandika kwa hati za Kirumi. Kijumwa alizitimiza vizuri shughuli za ufisiri na hizo za unukuzi akisaidiwa mno na vipawa vyake vya kujua vyema lugha ya Kiarabu na ya Kiswahili, kujua vizuri matumizi ya hati za Kiarabu na za Kirumi na zaidi kuwa na mkono mzuri wa maandishi.

Kijumwa ni manju ambaye alijua Kiarabu na pia alijifunza kuandika Kiswahili kwa hati za Kirumi. Ujuzi huu ndio ulimfanya Kijumwa aonekane msaidizi mkubwa wa watafiti hawa. Zifuatazo ni baadhi ya nakala alizozinukuu na kuwapa watafiti waliokuwa wamemtaka awafanyie hivyo:

Utendi wa Mwanakupona

Huu ni utenzi ambao ilitungwa na Mwanakupona Mushamu. Kijumwa aliunakili kwa hati za Kirumi kutoka hati za Kiarabu na kumpa Alice Werner mwaka 1911 na W. Hichens mwaka 1912. Pia aliwapatia Prof. Meinhof, H. Lambert na Capt. Stigand. Kijumwa alikuwa na nakala mbili za utenzi huu. Nakala ya kwanza ilitoka Siu na nakala ya pili ilitoka Lamu ambayo aliipata kutoka kwa Mwenye (Mwinyi) Mansabu Allen (1971) anasema mmoja wa wale waliopatia nakala ya Utendi wa Mwanakupona ni Mohammed Kijumwa, na kwamba nakala hii, ikiwa katika maandishi ya mkono wa Kijumwa inapatikana katika (Harvard African Studies).

Shairi la Liyongo

Kuhusu Liyongo, kuna kazi tatu za fasihi ambazo zilinakiliwa na Kijumwa na kuwapa watafiti. “Takhmisa ya Liyongo” ni shairi alilolinakili Kijumwa na

kuwapa Alice Werner na Prof Meinhof. Hawa walichapisha shairi hili mwaka 1924 na 1925. Mnamo mwaka 1933, Kijumwa alimtafsiria na kumwandikia W. Hichens shairi hilo la "Takhmisa ya Liyongo." Katika mwaka 1936, Kijumwa alimnakilia E. Dammann shairi la Liyongo. Utendi au Hadithi ya Liyongo haimo katika tapo hili kwa sababu aliutunga yeye mwenyewe Kijumwa. Aidha kuna shairi la Liyongo Fumo alilonakili Kijumwa kutoka kitabu cha mzee bin Mahadhoo (Abouegl ,1984).

Utendi wa Ayubu

Huu ni mmoja wa tenzi za kale na unakisiwa ya kwamba una miaka karibu 200 tangu utungwe. Kijumwa aliutafsiri na kuunakili utenzi huu na kumpatia A. Werner mwezi Septemba, mwaka 1913. Werner hakuwa anajua Kiarabu kwa hivyo alitegemea sana usaidizi wa watu ambao anawataja kama vile Mohammed bin Abubakari bin Umari Kijumwa al Bakari ambaye alijulikana kama Mohammed Kijumwa. Nakala ya Werner ya Utendi wa Ayubu umeandikwa kwa mkono na Mohammed Kijumwa ambao una tarehe ya mwaka wa 1913 (Allen, 1971). Werner aliuchapisha utenzi huu mwaka 1921, katika gazeti la *Mamboleo*, Dar-es-Salaam (Abouegl, 1984).

Uunguo Maneno ya Miraji

Ni shairi ambalo Kijumwa alitafsiri na kuliandika kwa hati za Kirumi na kumpa A.Werner. Vile vile alimpelekea A.Werner tafsiri ya Miraji iliyotokana na vitabu viwili vya Kiarabu:

Al-Israi Wa-al-miiraji Li-al-Hawa Nabiy, kilichoandikwa na Abdu Allah Ibn Abba na *Hawa Nuzhat-al-Majalis wa Muntakhab al-Nafais*, kilichoandikwa na Abdu ar-Rahman as-Safuriy al-Shafiiy.

Al-Inkishafi

Huu ni utenzi mashuhuri uliotungwa na Sayyid Abdalla bin Ali bin Nassir (1720-1820). Kijumwa alitoa nakala ya utenzi huu na kuwapatia W. Hichens, A.Werner, Prof Meinhof na Capt. Stigand. Kijumwa alikuwa na nakala za aina mbili za utenzi huu. Nakala ya kwanza ni ya zamani kutoka kwa Mwenye Mansabu wa aila ya al-Hassainiy. Nakala hii aliywapa watafiti hao ndiyo inayojulikana hivi sasa kama nakala ya kaskazini ya utenzi huu wa Inkishafi. Hichens (1972) anasema alipata nakala ya Inkishafi iliyandoikwa 1910 na Mohammed (Kijumwa) Abubakar bin Umar al-Bakary, mtunzi na msafiri mashuhuri wa Lamu.

Utenzi wa Tabaraka

Huu ni utenzi unaohusu sura mbili katika Koran. Utensi huu ultafsiriwa na mwalimu wa Kijumwa, Mwenye Mansabu, lakini ni Kijumwa ndiye aliyempatia utenzi huu, Bi. Alice Werner.

Utendi wa Kutawafu Muhammed

Kijumwa alitafsiri na kunakili *Utenzi wa Kutawafu* na kumpa E. Dammann, mwaka 1938. Pia alimpatia J. W. Allen na Dr. Buttner ambaye aliuchapisha.

Utendi wa Mikidadi na Mayasa

Huu ni utenzi unaopatikana katika fasihi simulizi ya Kiarabu. Ultafsiriwa na kunakiliwa na Kijumwa na kumpatia A. Werner, mwaka 1918, ambaye aliuchapisha mwaka wa 1932. Werner (1932) anasema, kuhusu Utendi wa Mikidadi na Mayasa, kuwa alipata usaidizi mkubwa kutoka kwa Mohammed Kijumwa wa Lamu na anamshukuru sana kwa kumpatia pia nakala ya awali zaidi ya utenzi huu.

Utendi wa Ngamia na Paa

Utenzi huu aliwapa W. Hichens, A. Werner na E. Dammann, Dammann ndiye aliuchapisha utenzi huu mwaka wa 1940. Allen (1971) anasema, School of Orient and African Studies, ina nakala ya Utendi wa *Ngamia na Paa* ambao umeandikwa kwa mkono wa Mohammed Kijumwa.

Kishamia

Ni utenzi ambao ultitungwa na Mwenye Mansabu. Ulinakiliwa na Kijumwa na kumpatia E. Dammann katika mwaka wa 1936 ambaye aliuchapisha, mwaka 1940. Utensi huu una beti 38.

Fahali

Hili ni shairi lililotungwa na Mahfudhi kutoka Siu. Lina beti 13. Kijumwa alilinakili na kumpatia E. Dammann aliyelichapisha, mwaka 1940.

Utendi wa Herekali

Utenzi huu ulijulikana pia kama *Chuo cha Herekali*, hasa katika sehemu za Mombasa. Huu ni utenzi wa zamani sana ambao una beti 1150. Kijumwa aliunakili kwa hati za Kirumi na kumpatia E. Dammann mnamo mwaka 1937. Alimpatia pia J.W. Allen.

Mzigo

Ni shairi lilitotungwa na Ali Koti wa Pate. Shairi hili lilinakiliwa na Kijumwa na kumpa W. Hichens.

Wajiwaji

Huu ni utenzi aliounakili Kijumwa na kumpa W. Hichens mnamo mwaka wa 1936. W. Hichens ndiye aliyeuchapisha utenzi huu. Kijumwa alikuwa akilipwa kwa kazi hizi zote za ufasiri na unukuzi wa kazi za fasihi alizowafanyia watafiti hawa wa Kizungu.

11.0 Kijumwa kama mtunzi

Mohammed Kijumwa alikuwa na kipaji cha sanaa za aina nyingi. Kipaji na ufundi alioibuka nao ulimfanya aitwe “Fundi” katika jumuiya yake ya Lamu nyakati hizo. Ufundu huu ulionekana zaidi hasa katika utunzi baada ya Bwana Langenbach kumfundisha Kijumwa jinsi ya kusoma na kuandika kwa hati za Kirumi (Abouegl, 1984).

Katika utunzi wake, Kijumwa alitanda katika tenzi, mashairi, nyimbo na hadithi fupi. Wale waliomjua, kama vile H. Lambert, walimweleza Kijumwa kama fundi mvumilivu mwenye umbuji wa hali ya juu katika utunzi. Alice Werner (1932) naye alimweleza Kijumwa kama mtunzi aliyebungu na kutunga kazi nyingi za fasihi. Allen (1971) anamtaja Kijumwa kama mtunzi wa shairi la “Mkonumbi”.

Kijumwa alikuwa msomi vile vile. Alichukua Koran na Hadithi za mtume Mohammed S.A.W kama msingi wa utunzi wake. Alisoma pia vitabu kadha wa kadha ambavyo kutoka kwavyo alipata tenzi, mashairi na hadithi na kutafsiri na kuziingiza katika fasihi ya Kiswahili. (Allen, 1971).

Nyingi ya kazi zake zinamulika imani ya dini ya Kiislamu pamoja na hali halisi ya maisha na mazingira ya Lamu. Vile vile baadhi ya tungo zake zinadhahirisha utamaduni wa Kiarabu ambao aliasoma katika vitabu kadha wa kadha vya Kiarabu. Baadhi ya tungo zake ni hizi:

Shairi la Wanawake wa Kiamu

Hili ni shairi lenye beti 19. Katika shairi hili, Kijumwa anawasifu wanawake wa Lamu kwa uzuri wao wa umbo, tabia na sura. Baadhi ya beti za shairi hili ni:

Babukheti kaazime hima mbawa za kipungu

Uje hapa nikutume nikupe maneno yangu

Nina mambo yanivume ya ndani mwa moyo wangu

Yaniwelee utungu kuwa ni mbali na Amu

Amu kuna wake ‘ali wa haiba na urembo
Nyama yao ya muili tabia na lao umbo
Mkindani hukubali hapati kunena yambo
Huwapati penye kombo wanawake wa Kiamu

Mwanamke wa Kiamu nyee zake akisuka
Maburudisho ya Shamu hali waridi kipaka
Kikaa kitini huramu hung’ara kimemetuka
Mwenye hasira huteka kwa wanawake wa Amu.

Tungo nyingine alizotunga Kijumwa ni:

Utendi wa Nana Werner

Huu ni utenzi aliotunga Kijumwa juu ya sifa na matendo ya A. Werner. Aidha kuna shairi aliloliita “Alice Werner” ambalo alilitunga kwa heshima yake baada ya kuombwa kufanya hivyo na W. Hichens wakati Werner alipokufa, mwaka 1935. Shairi hili lilimfikia Hichens Februari, mwaka 1936 na lina beti 22.

Utendi wa Safari

Huu ni utenzi unaozungumzia safari ya E. Dammann na mumewe ya kutembelea miji ya Matondoni, Pate na Malindi. Utendi huu alimpa E. Dammann, mwaka 1936 ambaye aliuchapisha, mwaka 1940.

Baadhi ya tungo nyingine nyingi alizotunga Kijumwa ni hizi:

Alika kama Harusi

Utendi wa Yusufu

Ushuhuda au Chuo cha Diraji

Utenzi wa Lamu

Kisa cha Kadhi

Utendi wa Nasara wa Arabu

Shairi la Fisi

Utamaduni wa Ndoa Lamu

Utendi wa Siraji – Huu ni utendi alioutunga kwa minajili ya kumuasa mtoto wake aliyeitwa Helewa.

Kuna tenzi na mashairi mengi ambayo yasemekana yalitungwa na Mohammed Kijumwa, lakini mwenyewe alidai yalitungwa na watunzi wengine. Jambo hili lilitokea kwa sababu watafiti Wazungu walikuwa wakimlipa kwa huduma aliyowapa ya kuwatafsiria na kuwaandikia tenzi na kazi za fasihi za watunzi waliomtangulia. Baadaye, Kijumwa aligundua ya kwamba Wazungu hao walikuwa wakimlipa zaidi kwa tungo ambazo zilikuwa si zake. Alikuwa akipewa mara mbili zaidi ya pesa zake za kutafsiri na kuandika utenzi huo na za

yule aliye kuwa akihifadhi utenzi huo. Alipogundua hivi, basi tungo nyingi alizikana akisema si zake ili alipwe pesa mara mbili – zake na za mtunzi au muhifadhi wa tenzi hizo. Sababu ya pili ya kuzikana baadhi ya tungo zake ni ya kisiasa. Kuna nyingine ambazo zilikuwa zikimwingilia kiongozi, hasa D.O. (District Officer) wa Lamu. Ujanja huu ulijulikana baadaye kwa sababu wengine, kama W. Hichens, alikuwa akimpelekea nakala Sheikh Hinawy wa Mombasa ili azipitie na atoe maoni. Huyu ndiye aliyefanya uchunguzi huko Lamu mpaka akagundua kuwa ni Kijumwa ndiye alikuwa mtunzi wa tungo hizo. Baadhi ya tungo alizozikana Kijumwa lakini inafahamika kuwa ndiye mtunzi ni hizi:

1. Shairi la Abdur Rahman na Sufiyani

Hili ni shairi alilolitunga Kijumwa na kudai lilitungwa na Liwazi aliye kuwa mwanamke wa kitumwa huko Lamu.

2. Utensi wa Mkunumbi

Huu ni utendi ambao aliwapelekea J.W. Allen na Lambert, mwaka 1913. Lambert aliuchapisha mwaka 1960. Allen (1971) anamrejelea Kijumwa kama mtunzi wa utenzi wa “Mkonumbi”.

3. Utendi au Hadithi ya Liyongo

Huu ni utenzi ambao unasemekana ulitungwa na Kijumwa kuhusu hadithi ya Liyongo Fumo.

4. Kisa cha Sayyidina Isa

Huu vile vile ni utenzi alioukana Kijumwa. Unazungumzia kisa cha Yesu kulingana na Koran na utamaduni wa Kiislamu.

12.0 Kijumwa kama mwalimu

Kijumwa alikuwa mwalimu wa Waswahili na Wazungu waliopenda kuboea katika utunzi wa nyimbo, tenzi na mashairi ya Kiswahili. Kijumwa alikuwa fanani ambaye hakuonea uchoyo elimu yake ya utunzi. Alijaribu sana kuwachotea wengine kipawa hiki kwa kuwafunza jinsi ya kutunga nyimbo, mashairi na tenzi. Baadhi ya wale waliokuwa wanafunzi wake ni Bwana Zena (Abouegl, 1984).

Bwana Zena alikuwa mwanafunzi wa Kijumwa katika utunzi wa nyimbo. Baadaye, Bwana Zena aliibuka kama mpinzani wa mwalimu wake katika mashindano ya ngoma na nyimbo. Mashindano haya yalikuwa kama pondo ya kuendeleza na kuweka utunzi wa nyimbo hai zaidi katika nyakati za Kijumwa.

Mwanafunzi mwingine ni Mbaruk kutoka Uguja. Baada ya kupata ujuzi wa kutunga nyimbo, Mbaruk aliungana na Siti binti Saad na kuunda kikundi chao cha ngoma ya Taarab huko Uguja (Abouegl, 1984). Wanafunzi wengine walikuwa ni Wazungu. Kijumwa aliwafunza hawa vageni lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Aidha aliwafunza jinsi ya kutunga mashairi ya Kiswahili. Mmoja wa wanafunzi hao ni H.E. Lambert. Baada ya kuhitimu, Lambert alikuwa mtunzi wa mashairi mpaka akachapisha diwani aliyoita Wimbo wa Kiebrania. Katika beti za kwanza, Lambert anamsifu Kijurwa (Mohammed Abu Umar al-Bakary) aliyemfundisha na kumfanya apende uhairi wa Kiswahili. Diwani hii ilichapishwa, mwaka 1959 (Abouegl, 1984).

13.0 Hitimisho

Umuhimu wa Kijumwa unaelezwa zaidi ra Allen akinukuliwa na Harris (1950) akisema ya kwamba Kijumwa alitenda nakubwa katika kuwaeleza wazungu fasihi ya Waswahili, alikuwa mwalimi na mfafanuzi kwa wasomi wengi wa Kizungu, kama vile Hichens Werner, Dammann, Lambert na wengine. Hata hivyo, Allen anadhania kuwa Kijumwa hakuwa mwaminifu kama mnukuzi. Pia anasema hakuwa manju kama watu vanavyomchukulia. Mbali na maoni haya, wasomi wengi kama vile Abdulaziż (1994), Harris (1950) na Shihabuddin (1973), wanamsifu Kijumwa kama nmoja wa mashaha wakubwa wa tungo za Kiswahili wa enzi zake.

Umashuhuri wake Kijumwa umefanya achukuliwe kama mwanafasihi aliyeendeleza fasihi ya Kiswahili kwa sababu alianzisha ngoma mbalimbali. Aliendeleza pia tenzi na ushairi wa Kiswahili kwa kutafsiri, kunakili na kuwapa watafiti tenzi na mashairi ya watunzi waliomtangulia. Watafiti hawa walichapisha tenzi hizo katika vitabu na majarida mbali mbali. Fauka ya hayo, Kijumwa mwenyewe alikuwa mtunzi wa tenzi na mashairi. Usanii wake unaweza kulinganishwa na wa Muyaka. Kijumwa anaweza kuchukuliwa kama Muyaka wa Lamu.

MAREJEÓ

- Abdulaziz, M.H. (1994) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi, Kenya Lit. Bureau.
- Abouegl, M.I (1984) "The Life and Works of Mohammed Kijumwa" unpublished Ph.D Thesis. University of London.
- Allen, J.W.T (1971) *Tendi* Nairobi. Heinemann.
- Dammann, E(1968/69) "Mohammad bin Abubekr bin Omar Kijumwa Masihi?" in Africa und Uberssee, L11 1968/1969 pg. 314-315.
- Grays, J(1957) *The British in Mombasa: 1824-1826*. London, Macmillan Pub.
- Hichens, W (1972) *Al- Inkishihi: The Soul's Awakening*. Nairobi. Oxford University Press.
- Knappert, J (1967) *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concepts of East African Islam as Reflected in the Utensi Literature*. Netherlands. Leiden Publishers.
- Mbele, J.L (1986) "The Liyongo Fumo Epic and Scholars" in *Kiswahili Journal* Vol. 53/1853/2, Dar-es-salaam, TUKI.
- Shihabuddin, C (1973) "Itangulizi wa Utensi wa Fumo Liyongo na Muhammed Kujumwa. Katika Kiswahili, TUKI, pg.iv.
- Mulokozi; M (1999) Ed. *Tensi Tatu za Kale*, Dar es Salaam, TUKI.
- Werner,A (1932) *The Story of Miqdad and Mayasa From the Swahili Arabic Text*. Medstead-Hampshire. The Azania Press.